

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO**

**14 MEI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 14 MEI, 2024**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa

Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **325. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara kutoka Kijiji cha Idete hadi Mgeta.

#### **326. MHESHIMIWA MARIAMU MADALU NYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Frank Weston - Tuwemacho - Namasakata hadi Misechela Tunduru.

**327. MHESHIMIWA GEOFFREY IDELPHONCE  
MWAMBE (MASASI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Mabweni na Mabwalo katika Shule za Sekondari za Marika, Temeke, Chanikanguo, Anna Abdallah na Mtandi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA  
MAZINGIRA):**

**328. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN  
(BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza Fukwe za Bahari zilizoathirika na maji upande wa Zanzibar.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**329. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS  
(BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha huduma za marekebisho kwa Watoto Wenye Ulemavu.

**WIZARA YA MAJI:**

**330. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni kwa nini Mradi wa Maji wa Kemondo – Maruku umechukua muda mrefu kukamilika.

**331. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha uchimbaji wa Visima vya Maji vilivyoanza kuchimbwa katika Jimbo la Tunduru Kaskazini.

**WIZARA YA AFYA:**

**332. MHESHIMIWA MOHAMMED SAID ISSA (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itakuwa na Hospitali Kuu ya Taifa moja ambayo itatoa huduma zote za afya bila kutegemea Hospitali nyingine.

**333. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini huduma ya *Ultrasound* itatolewa bure kwa Wajawazito wanapohudhuria Kliniki.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**334. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaweka taa Uwanja wa Ndege wa Mafia ili kuwezesha Ndege kubwa kupeleka Watalii kutembelea Kisiwa cha Mafia.

**335. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itahakikisha usalama wa Abiria na mali zao kwa Wasafiri wanaotumia Meli ya MV Victoria ndani ya Ziwa Victoria.

## **WIZARA YA MADINI:**

### **336. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, upi mpango wa kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa Vibali kwa Wachimbaji Wadogo na kutozwa mapato kwenye mchanga Mgodu wa Kebaga.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **337. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaweka wavu maeneo ambayo Wananchi wanapoteza maisha kwa kuliwa na Mamba wanapofuata maji katika Ziwa Tanganyika.

### **338. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaifanyia Marekebisho Sheria ya Kifuta machozi kwa madhara yanayosababishwa na Wanyamapori.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA**  
**14 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**

